02/12/2025

# TANGAZO LA NAFASI ZA AJIRA

## HOSPITALI YA WASSO – JIMBO KUU KATOLIKI ARUSHA

## WILAYA YA NGORONGORO

Hospitali ya Wasso ni hospitali ya kanisa jimbo kuu katoliki la Arusha inayotoa huduma za afya kwa jamii ya Ngorongoro na maeneo ya jirani.

Mganga Mfawidhi Hospitali ya Wasso anakaribisha maombi ya kazi kwa kada ya **Afisa Hesabu Daraja la II.**

### 1. **AFISA HESABU DARAJA LA II (ACCOUNTS OFFICER II)** NAFASI (1)

#### a) SIFA ZA MWOMBAJI

- Awe na Shahada ya Uhasibu, Fedha, Uchumi au fani inayohusiana kutoka chuo kinachotambuliwa na Serikali
- Awe mwenye CPA (T) au sifa nyingine inayolingana na kutambuliwa na Bodi ya Wahasibu na Wakaguzi (NBAA).
- Awe amesajiliwa na NBAA kama Certified public Accountant.
- Awe na ufahamu wa mifumo ya kifedha ya Serikali na Mifumo mingine ya Kiteknolojia ya uhasibu.
- Awe na uwezo mzuri wa kutumia kompyuta, hasa programu za uhasibu na MS Office (Word, Excel, Outlook).
- Awe na uzoefu au uelewa wa masuala ya fedha katika Sekta ya Afya.
- Awe na uwezo wa kufanya kazi kwa umakini, uadilifu, uaminifu na kwa kufuata taratibu za kifedha.
- Awe na mawasiliano mazuri, nidhamu, na uwezo wa kufanya kazi kwa kushirikiana na wengine.

#### b) MAJUKUMU YA KAZI

- Kuandaa na kutunza kumbukumbu za fedha za Hospitali kwa mujibu wa kanuni na taratibu.
- Kuhakikisha Mapato na Matumizi yote ya fedha yanarekodiwa ipasavyo kwenye mifumo ya uhasibu.
- Kuandaa hatimiliki, Vocha, Risiti, Malipo na nyaraka zote za kifedha.
- Kufanya upatanisho wa akaunti (Bank Reconciliation) kila mwezi.
- Kushiriki katika kuandaa bajeti ya mwaka, tathmini ya bajeti na taarifa za fedha za robo mwaka na mwaka mzima.
- Kuandaa na kuwasilisha taarifa za kifedha kwa uongozi wa Hospitali.
- Kufanya uhakiki wa madai kabla ya kufanyika kwa malipo.
- Kushiriki katika ukusanyaji na ufuatiliaji wa mapato ya Hospitali.

- Kuhakikisha uzingatiaji wa sera, sheria na kanuni za fedha za Serikali na Hospitali.
- Kushiriki katika Kufanya ukaguzi wa ndani na kusaidia ukaguzi wa nje unapohitajika,
- Kufanya majukumu mengine ya kifedha utakayopangiwa na mwajiri kulingana na taaluma yako.

**MASHARITI YA JUMLA**

i. Mwombaji awe ni Raia wa Tanzania na mwenye umri usiozidi miaka 45.
ii. Cheti cha mtihani wa kidato cha IV na VI.
iii. Mwombaji aambatishe nakala ya cheti cha kuzaliwa, Kitambulisho cha Taifa (NIDA) au kitambulisho cha mpiga kura.
iv. Mwombaji aambatishe maelezo binafsi yanayojitosheleza yenye anwani na namba za simu za kuaminika pamoja na majina ya wadhamini (Referees) watatu wa kuaminika.
v. **Testimonials, Provisional Results, Statement of Results, hati ya matokeo ya kidado cha nne na sita (FORM IV AND VI RESULTS SLIPS) HAVITAKUBALIWA.**
vi. **Mwombaji aliyesoma nje ya Tanzania ahakikishe cheti chake kimehakikiwa na kuidhinishwa na Mamlaka husika (TCU au NECTA).**
vii. Uwasilishaji wa taarifa na sifa za kughushi mhusika atachukuliwa hatua za kisheria.
viii. **Mwisho wa kutuma maombi ya kazi ni tarehe 31 Disemba, 2025.**
ix. **Maombi yawasilishwe kwa njia ya barua kwa Mganga Mfawidhi wa Hospitali ya Wasso S. L.P. 42, LOLIONDO, barua pepe. secretary@wassohospital.org.**

WASSO HOSPITAL P.O. Box 42 LOLIONDO ARCHDIOCESE OF ARUSHA

...............................................

Angela Joseph
**Kny: MGANGA MFAWIDHI**